

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA**

Simu Na: +255 (026) 2963630  
Nukushi: +255 (026) 2963629  
Barua Pepe: [ded@buchosadc.go.tz](mailto:ded@buchosadc.go.tz)  
Tovuti: [www.buchosadc.go.tz](http://www.buchosadc.go.tz)



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)  
S.L.P 44  
**BUCHOSA-SENGEREMA**

Unapojibu tafadhari taja:

**Kumb.Na. AB.208/117/01/42**

**03/11/2021**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa baada ya kupata kibali cha ajira mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, anatangaza nafasi za kazi kwa wananchi wa Tanzania wenye sifa na ujuzi wa kujaza nafasi ya **Mtendaji wa kijiji daraja la III (nafasi 3)**.

**a) Sifa za mwombaji:**

Kuajiriwa mwenye Elimu ya Kidato cha nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**b) Kazi na Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji:**

1. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
2. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
3. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji.
4. Katibu wa mikutano ya kamati zote za Halmashauri ya kijiji.
5. Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu.
6. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
7. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalamu katika kijiji.
8. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
9. Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo katika kijiji.
10. Kupokea, kusikiliza na katatua malalamiko na migogoro ya wananchi.

11. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji na

12. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

**c) MSHAHARA:**

Mtumishi atakayefanikiwa kuajiriwa katika nafasi hii, ataanza na mshahara wa TGS B.

**MASHARTI YA JUMLA**

1. Mwombaji lazima awe Raia wa Tanzania.
2. Awe na Umri wa miaka 18 hadi 45.
3. Awe mwadilifu na asiwe na historia ya uhalifu
4. Waombaji waambatishe nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo na vyeti vya kidato cha nne vilivyothibitishwa na wakili au mahakama
5. Testimonials, provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita(form iv na form vi result slip) havitakubalika
6. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika.

Mwombaji mwenye sifa anatakiwa kutuma maombi kwa anuani ifuatayo;

**Mkurugenzi Mtendaji,**

**Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa,**

**S.L.P. 44,**

**BUCHOSA – SENGEREMA.**

Mwombaji aambatishe katika barua ya maombi:- maelezo binafsi (CV), vivuli vya vyeti vya Elimu na Taaluma, cheti cha kuzaliwa cha mwombaji, na namba ya simu.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **17/11/2021 saa tisa na nusu mchana.**

NB:Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri [www.buchosadc.go.tz](http://www.buchosadc.go.tz), tovuti ya secretarieti ya ajira [www.ajira.go.tz](http://www.ajira.go.tz) na katika mbao za matangazo za Halmashauri.



Paulo Sostheness Malala

**Mkurugenzi Mtendaji (BUCHOSA) (W)**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
BUCHOSA**